

OFISI YA RAIS TAMISEMI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA  
SHULE YA SEKONDARI MT.MASUSA,  
S.L.P 82,  
LUDEWA.  
25/11/2020.

KUMB.NA.MMSS/KDT/VOL/

JINA LA MWANAFUNZI.....

S/M.....

LUDEWA.

**YAH;MAAGIZO YA KUJUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MT.MASUSA**

**WILAYA YA LUDEWA MKOA WA NJOMBE MWAKA 2021**

**1.0 UTANGULIZI.**

Ninayofuraha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021 .Shule ya sekondari Mt.Masusa ipo umbali wa km 11 magharibi mwa mji mdogo wa Mlangali Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa.

Usafiri wa mabasi unapatikana kituo cha mabasi Mlangali kwa nauli ya Tsh.2,000/=,muhula wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 15/01/2021 siku ya ijumaa.

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi hakikisha unamuandalia vitu vifuatavyo;

**2.1SARE ZA SHULE**

(a) Sare ya darasani pamoja na kwenye shughuli nyingine rasmi za shule.

-Wavulana.Suruali rangi ya bluu nyeusi(dark blue) pea 2

.Shati nyeupe mikono mirefu pea 2

.Viatu vyeusi vyta kufunga na kamba pea 2

.Soksi nyeusi/bluu joz 2

.Sweta rangi ya damu ya mzee shingo muundo wa V (kwaajili ya wakati wa baridi).

Wasichana.Suruali rangi ya bluu nyeusi(dark blue) mshono wa kawaida pea 2.

.Blaus i nyeupe mikono mifupi aina ya kisoro pea 2 (mshono umeambatanishwa).

.Viatu vyeusi nya kufunga na kamba pea 2.

.Soksi nyeupe jozi 2.

.Sweta rangi ya damu ya mzee shingo muundo wa V (kwaajili ya wakati wa baridi).

(b) Sare za michezo

.Wavulana .T sheti(fulana) rangi ya bluu, bukta rangi yeyote na raba au viatu nya michezo.

.Wasichana.Track suit nyeusi yenye michirizi myeupe na raba au viatu nya michezo.

NB.aina ya kitambaa kwa Wasichana na Wavulana imeambatanishwa hapo juu.

2.2 Vifaa nya darasani.

Daftari kubwa kaunta 10 na ndogo 10,kalamu za wino bluu au nyeusi pamoja na kalamu ya risasi(penseli) na mkebe wenye vifaa.

2.3 Chakula kwa Wanafunzi

Kwa upande wa chakula cha mchana Wanafunzi wote wanahusika lakini chakula cha jioni ni Wanafunzi wa Hosteli tu.

2.4.Huduma ya Hosteli

Nafasi nya kuishi Hosteli ni kwa Wasichana tu na ni wale wa vidato nya mitihani.

**3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.**

3.1 Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995.Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Waziri mkuu TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi wa uendeshaji Elimu.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shulenii.

(a)Heshima kwa viongozi ,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni lazima.

(b)Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni lazima.

(c)Kushirikiana kwa makini kufanya Maandalio ya jioni(evening preparation).

(d)Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

(e)Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo.

(f)Kutunza usafi wa mwili ,mavazi na mazingira ya shule.

(g)Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

(h)Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

(i)Kutunza mali za shule.

3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.

(a) Wizi

(b) Uasherati na ushoga.

(c)Ubakaji

(d)Ulevi na matumizi ya Madawa ya kulevya kama vile bangi,cocaine,mirungi,kubeli na kadhalika.

(e) Kupigana au kupiga.

(f) Kuharibu kwa makusudi mali za umma.

(h)Kuwa mjamzito /kupata mimba.

(i) Kuoa au kuolewa.

(j) Kutoa mimba.

(k) Kugoma , kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvurunga amani na usalama wa shule au Watu.

(l)Kukataa adhabu kwa makusudi.

(n)Kuwa na simu ya mkononi.

#### **4.0Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shulenii na Mwanafunzi siku ya kuripoti.**

(a) Medical Examination form ambayo inajazwa na Mganga mkuu wa Hospitali au Zahanati ya serikali.Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti.

(b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutii sheria za Shule.Fomu hii ijazwe kikamilifu na Mzazi pamoja na Mwanafunzi.

NB.Fomu zilizotajwa hapo juu zimeambatanishwa mwishoni mwa barua hii.

5.0Tafadhali soma kwa makini maelekezo /maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA MT.MASUSA SEKONDARI.**

**OFISI YA RAIS –TAMISEMI**

**SHULE YA SEKONDARI MT.MASUSA**

**FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MT.MASUSA**

**A.SEHEMU YA MWANAFUNZI**

1. Mimi.....msichana/mvulana nimekubali kuingia kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Mt.Masusa kama Mwanafunzi wa Hosteli/Kutwa tangu tarehe...../...../2021 nitafika bila kukosa.

2. Nitatii sheria za shule na kanuni zote ,na nitakuwa Mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za kujitegemea.

Sahihi ya Mwanafunzi.....Tarehe.....

**1.MAONI YA MZAZI /MLEZI KUHUSU MTOTO**

Tafadhalii eleza endapo kuna tatizo ,jambo au tabia yoyote ambayo Mkuu wa Shule anapaswa kufahamu juu ya Mtoto wako.

.....  
.....  
.....  
.....

**2.UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI**

Nimesoma maelezo yote na kuyaelewa vema.Hivyo nakubali kutekeleza maagizo yote kikamilifu.Pia Mwanagu kufuata na kuzingatia taratibu zote za shule.

Jina la Mzazi/Mlezi.....sahihi.....tarehe...../...../2021